**Tanzania Human Rights Defenders Coalition [THRD-Coalition]**

**P. O. Box 75254 Dar es Salaam, TANZANIA Telephone: +255-22-2773038/48, Fax: +255-22-2773037, Mob: +255 783 172394 E-mail: defenderscoalition@rocketmail.com**

# TAMKO KWA UMMA JUU YA HALI YA WATETEZI WA HAKI ZA WAFUGAJI LOLIONDO

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) unalaani vikali kutishwa kwa watetezi wa haki za wafugaji walioko Loliondo ambao kwa muda mrefusasa wamekua wakifanya uhamasishaji wa haki ya ardhi kwa wafugaji baada ya wafugaji hao kupata misukosuko kutoka kwa wawekezaji waliokua na nia ya kuwanyang'anya ardhi.

Vitisho kwa watetezi wa haki za wafugaji wakiwemowaandishi wa habari, havijashuhudiwa loliondo tu bali hata maeneo mengine ya nchi ambayo yana idadi kubwa ya wafugaji kama vile Kiteto, Hannang, Kilosa, Morogoro, Mbeya, Mara, na rukwa na sababu moja wapo ni uwepo wa wawekezaji katika maeneo hayo.

Kuna Asasi 17 Loliondo ambazo zinafanya kazi kwa nguvu zote katika kuhakikisha haki ya ardhi kwa wakulima inalindwa, ni jambola kushangaza kuona kuwa Asasi zote hizo zimekua zikituhumiwa mara kwa mara na serikali kuwa zinahamasisha migogoro ya Ardhi swala lililopelekea baadhi ya vyombo vya habari kuandika vibaya kuhusu vingozi wa asasi hizo bila ya kuwa na tafiti za kutosha.

Baadhi ya Asasi na viongozi walizopokea vitisho ni; Ngorongoro NGOs Network(NGONET), Inayoongozwa na Samweli Nanghiria, UJAMAA Community Resources Trust(U-CRT) ambayo mratibu wake ni Makko Kondei, PWC inayoratibiwa na Joseph Melau Alayce, ACORD iliyochini ya uongozi wa Lokola Ndibalema, PALISEP inayoongozwa na Robert Kamakia pamoja na LASHEHABINGO iliyo chini ya uratibu wa Charles ole Ndangoya.

Asasi zingine zilizotuhumiwa kwa kuchochea migogoro ya ardhi huko lolindo ni pamoja na RAMAT inayoratibiwa na Yanic Ndoinyo, MACAO inayoratibiwa na Baraka Eliud, AMBUDEO ambayo mratibuwake ni Joseph Kashe, PCF chini ya uongozi wa Joseph Parsambei and Ngorongoro positive Support inayoratibiwa na Alfred Mabula.
Ni ukweli usiopingika kwamba waandishi wa habari pamoja na watetezi wengine waliokuwa mstari wa mbele kufichua vitendo vya uvunjifu wa haki ya ardhi huko loliondo wamekua wakipokea vitisho kufikia wakati wengine wamekua wakituhumiwa kuwa sio watanzania.

Watetezi wa wafugaji huko loliondo hivi karibuni walipigwa na butwaa kutambua kuwa serikali za mitaa ziliamua kufumbia masikio amri iliyotolewa na Waziri Mkuu MizengoPinda aliyointoa mnamo

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Board of Directors:
Dr. Helen Kijo Bisimba, Harous Mpatani, Martina Kabisama, Kenneth Simbaya, Joseph Parsambei, Saed Kubenea, Michael Kyande, Vicky Ntetema and Ernest Kimaya.

tarehe 23 Septemba 2013, kuwa wakazi wa Loliondo wasinyang'anywe ardhi na waendelee kudumisha tamaduni yao ya ufugaji katika eneo hilo kutokana na kitendo hiki waziri mkuu aliwasaidia watanzania zaidi ya elfu nane wanaoishi katika vijiji vinane vinayozunguka misitu ya loliondo.

Mtandao unawatambua watetezi wote ambao bado wanaendelea kutishiwa kutokana na kupaza sauti zao kupinga migogoro ya ardhi mmoja wao akiwa ni Samweli Nangirwa, ambaye aliwekwa kizuizini na kuhojiwa katika kituo cha polisi kwa zaidi ya masaa manne mnamo tarehe 4 Desemba 2014. Mtandao unalaandi vikali kuhojiwa kwa muda mrefu kiasi hiki kwani inapelekea manyanyaso.

Mnamo siku hiyohiyo mwandishi wa habari kutoka Aljazeera-Nairobi, Emiy Johnson aliwekwa kizuizini na kupewa masaa kumi na mbili ya kuondoka Loliondo ingawa alikuwa na vithibitisho muhimu vya kufanya kazi ya uandishi nchini na kwa muda husika. Wengine walioonja tishio la vitisho ni waandishi watano wa hapa nchini. Vitisho hivi vilikuja baada ya uandaaji wa kikao halali kwa ajili ya wakazi wa Loliondo kilichohudhuriwa na wafugaji 2000 waliodhamiria kuzungumzia migogoro ya ardhi, na matatizo wanayoyapata kutoka kwa wawekezaji kuu likiwa ni kunyang'anywa kwa ardhi.

Mtandao unatambua ya kwamba baadhi ya vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu nchini zikiwemo haki za watetezi wa haki za binadamu vingeweza kuzuiliwa kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG) ingekuwa na viongozi wajuu. Itambulike ya kwamba ni karibu mwaka sasa tangu Tume kufanya kazi bila ya kuwa na Mwenyekiti, Mwenyekiti msaidizi na makamishna wengine; hivyo basi bila uongozi huo ni sawa na hakuna tume.

Mwenyekiti na mwenyekiti Msaidizi wa tume ni viongozi wanaoteuliwa na Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana a mapendekezo ya kamati ya uteuzi chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 kifungu 129(2)(a)&(3), kipengele namba 7 cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, No. 7 ya 2001.

**WITO:**

1. Jeshi la polisi lifanye utafiti kuhusu tuhuma wanazotupiwa watetezi wa haki za wafugaji ikiwemo na waandishi wa habari. Watetezi wa haki ni watu ambao wao au pamoja na wengine huhamasisha au/na kulinda haki za binadamu. Hivyo kutokana na Tamko la Watetezi wa Haki za Binadamu la mwaka 1998 watetezi wanatakiwa kulindwa.

2. Mtandao unawasihi wahanga wa vitisho hivi kufanya juhudi za jihada kujilinda na maadui wa haki kwa ajili ya usalama. Mtandao unaamini kuwa mchango wa watetezi ni wa muhimu sana na hivyo maisha yao ni ya muhimu pia.

3. Mtandao unamsihi rahisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Jakaya Mrisho Kikwete kutumia mamlaka yake kuteua Mwenyekiti wa Tume na viongozi wengine waliobaki ili kuipa nguvu tume kwa ajili ya kuhamasisha na kulinda haki za binadamu nchini.


Board of Directors:
Dr. Helen Kijo Bisimba, Harous Mpatani, Martina Kabisama, Kenneth Simbaya, Joseph Parsambei, Saed Kubenea, Michael Kyande, Vicky Ntetema and Ernest Kimaya.

**Imetolewa na;**
**ONESMO OLENGURUMWA**
**Mratibu wa Mtandao,**
**Tanzania Human Rights Defenders Coalition (THRDC)**

THRD-Coalition

Board of Directors:
Dr. Helen Kijo Bisimba, Harous Mpatani, Martina Kabisama, Kenneth Simbaya, Joseph Parsambei, Saed Kubenea, Michael Kyande, Vicky Ntetema and Ernest Kimaya.